Government of **Western Australia**
**Mental Health Commission**

## Una haki ya:

- kupokea maelezo kuhusu haki zako na kupata majibu kwa maswali yako
- uchunguzi wa kimwili baada ya kulazwa hospitalini
- mahojiano na mtaalum wa magonjwa ya akili
- kuteua mtu aliyeteuliwa
- mpango wa matibabu, msaada na kuruhusu
- kuwasiliana na watu kwa posta, simu, au baruapepe, na kutembelewa (haki hii inaweza kuwa na mipaka)
- ufaragha na usiri
- kufikia makumbukumbu yako ya uganga (haki hii inaweza kuwa na mipaka)
- kutunza mali yako ya kibinafsi kwa salama wakati umo hospitalini
- maoni ya ziada kutoka mtaalum mwengine wa magonjwa ya akili – unaweza kumwombea mtaalum wako wa magonjwa ya akili, au Mtaalum Mkuu wa magonjwa ya akili (s: 9222 4462) ili kupanga hiyo
- kufikia Huduma ya Utetesi wa Afya ya Akili (s: 1800 999 057). Mtetesi wa afya ya akili atakuwasiliana nawe bila kufikiri katika siku 7 (masaa 24 kwa watoto) baada ya wewe kuwa mgonjwa asiyekusudiwa
- kutoa malalamiko kwa huduma ya afya ya akili. Unaweza pia kulalamika kwa Ofisi ya Malalamiko ya Huduma za Afya na Ulemavu (HaDSCO) (s: 1800 813 583).
- kupata kesi zako kukaguliwa rasmi na Baraza ya Afya ya Akili (s: 08  6145 3900). Baraza itapanga usikilizaji katika wiki 5 (siku 10 days kwa watoto) baada ya wewe kuwa mgonjwa asiyekusudiwa.

## Maelezo zaidi

Maelezo katika brosha hii inahusisha masheria ambayo yamo Sheria ya Afya ya Akili 2014. Maelezo kuhusu Sheria hii imefupishwa katika seti ya brosha zifuatazo:

- Kupendekezwa kwenda kwa mtaalum wa magonjwa ya akili kwa uchunguzi
- Maagizo ya matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa hospitalini
- Maagizo ya matibabu ya jamii
- Maelezo kwa wagonjwa wa hiari
- Kupokea matibabu kwa ugonjwa wa akili
- Maelezo kwa watu wanaosaidia kibinafsi
- Watu walioteuliwa: Jinsi ya kuteua na maana kwake.

### Brosha zingine zinapatikana kutoka:

- Baraza ya Afya ya Akili
- Huduma ya Utetesi wa Afya ya Akili
- Kituo cha Sheria ya Afya ya Akili.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Sheria ya Afya ya Akili 2014 na nyenzo zingine, angalia tovuti ya Tume ya Afya ya Akili: www.mhc.wa.gov.au au pigia simu (08) 6272 1200

This document can be made available in other languages and alternative formats on request.

Published by the Mental Health Commission (2015)

# Maagizo ya matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa



Agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa (Fomu 6A au 6B) ni agizo chini la Sheria ya Afya ya Akili 2014 ili upokee matibabu kama mgonjwa asiyekusudiwa hospitalini.

Brosha hii inakupa maelezo kuhusu haki zako ni nini na unachoweza kutazamia kama upo na agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa.

## Kwa nini agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa lilifanyikwa?

Kama wewe upo na agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa (Fomu 6A au 6B) hivi ni kwa sababu mtaalum wa magonjwa ya akili alikuchunguza na ameamuliwa kuwa:

- una ugonjwa wa akili unaohitaji matibabu,
- kuna hatari ya maana kwako mwenyewe au kwa mtu mwengine kama hupati matibabu,
- huna afya ya kutosha kuweza kuamua uamuzi kuhusu matibabu,
- matibabu katika jamii sio uchaguzi unaofaa kulingana na hali, na
- hakuna njia yenye mipaka kidogo zaidi ya kukupa matibabu badala ya agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa.

## Agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa lina maana gani kwako?

Agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa lina maana kuwa:

- utalazwa hospitali inayotajwa katika agizo,
- utapokea matibabu kwa ugonjwa wako wa akili pale hospitali ileile, na
- hutaruhusiwa kuondoka hospitali mpaka agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa linaisha (au isipokuwa unakubaliwa ruhusa)

Tofauti kati ya Fomu 6A na 6B ni aina ya hospitali unayolazwa.

Fomu 6B itatumika ukiwa afya yako ya kimwili ni hatari kali na unahitaji kuwemo hospitali inayoweza kutiba hali yako ya kimwili.

## Je, unapata nafasi kuamua matibabu unayopokea?

Utaombewa kwa ruhusa yako kila mara (makubaliano) kabla kupewa matibabu. Lakini, kuwa mgonjwa asiyekusudiwa kuna maana kuwa ikihitajika, unaweza kupewa matibabu bila ruhusa yako. Timu yako ya tiba itafikiria matakwa yako wanapoamua maamuzi kuhusu matibabu unayopata na utahusishwa pia katika kupanga mpango wako wa matibabu, msaada na kuruhusu.

## Unaruhusiwa kuondoka hospitali?

Sio lazima utakaa wadi iliyofungwa, lakini, huwezi kuondoka hospitali bila ruhusa. Ukiwa unaondoka, mfanyakazi, afisa wa usafiri au polisi anaweza kukurudisha hospitalini.

Unaweza kumwomba mtaalum wako wa magonjwa ya akili kwa ruhusa kutoka hospitali. Mtaalum wa magonjwa ya akili anaweza kukubali ikiwa kutasaidia kupata nafuu yako tena na ni usalama kwa wewe kuwa nje hospitali. Yeye azungumze na mtunzaji/familia yako kwanza. Urudi hospitalini wakati ruhusa yako inapomaliza. Usiporudi, mfanyakazi, afisa wa usafiri au polisi anaweza kukuchukua kurudi hospitalini.

## Agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa linaendelea kwa muda gani?

Agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa linaweza kuendelea kwa hadi ya **siku 21** kwa watu wazima au **siku 14** kwa watoto (chini ya umri wa 18).

Katika wiki ya mwisho wa agizo, mtaalum wa magonjwa ya akili atakuchunguza tena na kuamua kama agizo linahitaji kuendelea. Mtaalum wa magonjwa ya akili anaweza kuendeleza agizo kwa hadi ya **miezi 3** kwa watu wazima na **siku 28** kwa watoto. Agiza linaweza kuendelea mara nyingi inavyowezekana kuhitajika mpaka una afya ya kutosha kutohitaji matibabu yasiyokusudiwa hospitalini.

## Agizo la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa linaisha jinsi gani?

Kwa wakati wowote unapokuwa mgonjwa, mtaalum wa magonjwa ya akili anaweza kuamua kuwa:

- huhitaji tena kuwa mgonjwa asiyekusudiwa na unaweza kokote kuendelea kuwa mgonjwa wa hiari au kuondoka hospitali, au
- unaweza kupokea matibabu sasa katika jamii kwa agizo la matibabu ya jamii.

Lazima uruhusiwe kuondoka hospitali kama:

- agizo lako la matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa linaisha na haliendelee, au
- Baraza ya Afya ya Akili inakagua kesi yako na inaamua kwamba huhitaji tena kuwa mgonjwa asiyekusudiwa hospitalini.